# HOTUBA YA MGENI RASMI BI. THERESIA MBANDO KWENYE UFUNGUZI WA MKUTANO WA TISA WA BARAZA LA WAFANYAKAZI LA TAASISI YA ELIMU YA WATU WAZIMA TAREHE 10 MEI 2018 DAR ES SALAAM

***Ndugu Mwenyekiti wa Baraza la Wafanyakazi la TEWW, Dkt. Kassimu Nihuka;***

***Mjumbe wa THTU Taifa;***

***Mjumbe wa Kamati Tendaji ya RAAWU Kanda ya Mashariki;***

***Katibu wa Baraza la Wafanyakazi TEWW;***

***Wajumbe wa Baraza;***

***Wageni waalikwa;***

***Waandishi wa habari;***

***Mabibi na Mabwana;***

Awali ya yote niwashukuru kwa kunialika siku hii ya leo kuja kufungua mkutano huu wa tisa wa Baraza la Wafanyakazi wa Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima. Pili niwapongeze menejimenti ya Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima kwa kuitisha kikao hiki cha Baraza la wafanyakazi ambacho ni matakwa ya sheria na kanuni zinazosimamia uendeshaji wa Taasisi za Umma kama hii ya kwenu. Hii ni ishara ya uongozi bora na haina budi kuendelezwa kwa ustawi wa Taasisi na wafanyakazi kwa ujumla.

**Ndugu Mwenyekiti;**

Napenda nitumie nafasi hii kumpongeza aliyekuwa Mwenyekiti wa Baraza la Wafanyakazi na Mkurugenzi wa Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima, Dkt. Fidelice Mafumiko aliyeteuliwa na Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kuwa Mkemia Mkuu wa Serikali. Hili ni jambo la kujivunia na inadhihirisha umahiri wenu katika kuchapa kazi na umakini mkubwa mlio nao katika kutekeleza majukumu yetu. Nawapongeza sana na nawasihi muendeleze kuchapa kazi. Vile vile, napenda nimpongeze Mwenyekiti mpya wa Baraza la wafanyakazi ambaye pia ni Kaimu Mkurugenzi wa TEWW Dkt. Kassimu Nihuka. Ni imani yangu kuwa "viatu" alivyokuachia Dkt. Mafumiko vimekutosha na kwamba utaendeleza mazuri yote aliyoanzisha mtangulizi wako kwa manufaa na ustawi wa Taasisi.

**Ndugu Mwenyekiti, Wageni Waalikwa na Wajumbe wa Baraza;**

Baraza la wafanyakazi ni takwa la kisheria na ambalo linawezesha Taasisi kufanya kazi zake kwa ufanisi na kwa uwazi bila migogoro baina ya wafanyakazi na Menejimenti. Baraza la Wafanyakazi ni chombo kinachorahisisha utendaji kazi mahala pa kazi na hivyo basi likiwa madhubuti, Taasisi husika na yenyewe itakuwa madhubuti. Hivyo ni jukumu lenu wajumbe kuhakikisha kwamba maoni, ushauri na mipango ya Baraza hili vinachangia katika kuleta maendeleo ya Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima na kuisaidia serikali ya Awamu ya tano kufikia malengo iliyojiwekea katika sekta ya elimu nchini. Vikao vya Baraza la Wafanyakazi kama hivi vinasaidia kujenga uhusiano mzuri kati ya wafanyakazi na Menejimenti na huleta mafanikio makubwa pale vinapotumika vizuri.

Ninaamini kabisa kuwa kupitia Baraza hili, dukuduku na changamoto zinazowakabili wafanyakazi zitawasilishwa kinagaubaga kupitia wajumbe wa mkutano huu ambao ni wawakilishi wa wafanyakazi wote wa Taasisi. Nitoe rai kuwasihi mjadiliane katika umoja na uwingi wenu huu kwa maslahi ya Taasisi. Tofauti za vyama vyenu vya wafanyakazi isiwagawe bali iwafanye muwe wamoja zaidi. Ni muhimu ajenda za Mkutano huu zikajadiliwa kwa mapana zaidi ili kutoa mwelekeo sahihi wa Taasisi ili nyote kama Taasisi mpate kujua mnakokwenda na jinsi ya kufika huko kwa mafanikio makubwa zaidi.

***Ndugu wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi,***

Binafsi naifahamu TEWW kwa miaka mingi kutokana na elimu ya kuinua kisomo pamoja na elimu kwa Umma kupitia madarasa ya kisomo na Kampeni zake mbalimbali. Nimefarijika kusikia kuwa mmeandaa Mkakati wa Kitaifa wa kuinua kisomo na elimu kwa Umma nchini. Naamini kuwa mkakati huu utachangia katika kupunguza tatizo la wasio jua kusoma na kuandika nchini kwani tatizo hili limekuwa likiongezeka mwaka hadi mwaka. Ushauri wangu kwa Taasisi ni

kuhakikisha fursa hiyo ya kisomo inaenda sambamba na fursa za kujifunza ujasiriamali na ufundi mbalimbali hasa katika viwanda vidogo vidogo.

***Ndugu Mwenyekiti,***

Nimefurahi kusikia kuwa mtatumia wanafunzi wenu katika kutoa na kuendesha kisomo nchini. Hili ni wazo zuri kwani linaendana na falsafa ya Baba wa Taifa, Mwalimu J.K. Nyerere yakuanzisha mafunzo ya elimu ya watu wazima. Baba wa Taifa alianzisha mafunzo ya elimu ya Watu wazima ili wahitimu waweze kushiriki katika kufundisha madarasa ya kisomo pamoja na kuelimisha jamii katika masuala mbalimbali ya kipaumbele kwda maendeleo ya Taifa na wananchi kwa ujumla. Nitoe rai kwenu kuendelea kupanua wigo na kuboresha programu za mafunzo mnayotoa ili kuandaa walimu na wawezeshaji wengi zaidi ili madarasa ya kisomo yasikose walimu. Inapendeza sana kusikia kuwa mmepanua wigo wa utoaji elimu kwa kuanzisha programu za Astashahada na Stashahada kwa njia ya Ujifunzaji Huria na Masafa kwani sasa watanzania wengi zaidi wataweza kujiendeleza hadi elimu ya chuo bila kulazimika kuhudhuria masomo kwenye vituo au kampasi zenu kwa muda wote wa masomo.

***Ndugu Mwenyekiti,***

Napenda nitumie nafasi hii kupongeza juhudi za menejimenti ya TEWW kwa juhudi mnazozifanya za kudurusu miongozo yenu mbalimbali ili iendane na mahitaji na matarajio ya mazingira ya sasa. Kama mnavyofahamu, dira ya serikali yetu ya awamu ya tano inayoongozwa na Rais John Pombe Magufuli ni kujenga Tanzania yenye uchumi wa kati unaotegemea viwanda. Hivyo ni budi miongozo na mipango mbalimbali ikaelekezwa katika kufikia lengo hili kubwa la Kitaifa. Ni imani yangu kuwa maboresho mnayoyafanya ya sheria iliyoianzisha Taasisi pamoja na kudurusu Mpango Mkakati wenu inalenga katika kuunga mkono ujenzi wa Taifa la uchumi wa kati wa viwanda pamoja na mambo mengine ya kipaumbele ndani ya Taasisi.

**Ndugu Mwenyekiti;**

Nimesikia katika hotuba yako kuwa mojawapo ya changamoto mlizo nazo ni uhaba wa fedha za ndani kutekeleza mipango yenu. Nimefurahi kusikia mikakati mbalimbali mnayoitekeleza ili kuongeza mapato ya Taasisi pamoja na kusimamia matumizi ya mapato hayo. Rai yangu kwda menejimenti na wajumbe ni kuwa suala hili ninaomba liwe ajenda yenu ya kudumu na isiishie tu kwenye Mkutano huu wa tisa wa Baraza la Wafanyakazi. Ni vyema mkahakikisha mikakati hii mliyokiwekea inawasaidia kuweza kuongeza pato la Taasisi ili kuboresha miundombinu, vitendea kazi na bila kusahau maslahi ya wafanyakazi. Kwa kufanya hivi mtaifanya Taasisi kuweza kusima kwa miguu yake yenyewe bila kuwa tegemezi kwa serikali au wadau mbalimbali wa maendeleo.

**Ndugu Mwenyekiti, Wageni Waalikwa, Wajumbe, Mabibi na Mabwana;**

Baada ya kusema hayo machache, nitangaze rasmi kuwa, sasa Mkutano wa tisa wa Baraza la Wafanyakazi wa Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima wa Mwaka 2018 umefunguliwa rasmi.

**ASANTENI SANA KWA KUNISIKILIZA**